



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Mtaa wa Kilimani,

S.L.P 1049, DODOMA,

Simu: +255 22 2135747/8; 0734 047 775

Faksi: +255 22 2111281

Barua Pepe: info@chragg.go.tz

Tovuti: www.chragg.go.tz

Februari 05, 2020

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inasikitishwa na kauli zinazotolewa na baadhi ya viongozi na makundi ya kisiasa na kijamii zinazoashiria uvunjivu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora nchini. Aidha, kauli hizo zimekuwa zikichochea kwa kiasi kikubwa wananchi kujichukulia sheria mikononi mwao kutokana na kutoridhishwa na vitendo vya baadhi ya wanasiasa.


Hivi karibuni kumesikika katika mitandao ya kijamii kauli mbalimbali zilizotolewa na baadhi ya watu wakitoa kauli za vitisho dhidi ya wengine kutokana na kutofautiana kimtazamo. Aidha, makundi mengine yamejitokeza kupinga hatua hiyo na kuahidi kuchukua hatua ambazo hazitoi sura nzuri katika ustawi wa misingi ya haki za binadamu na utawala bora nchini.

Kutokana na hali hiyo, Tume inapenda kusesitiza juu ya umuhimu wa kuvumiliana na kutumia taratibu za Kisheria katika kutafuta ufumbuzi wa masuala mbali mbali yanayolalamikiwa. Kauli hizi zisipodhibitiwa zinaweza kupelekea pia uvunjivu wa amani na utulivu tulio nao hapa nchini.

Tume pia inaviomba Vyama vya Siasa kusimamia na kuwadhibiti wafuasi wao kutotumia lugha ambazo zinaweza kupelekea uvunjivu wa haki za Binaadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Sote tusimame imara katika kupinga kauli hizo ili kudumisha amani na utulivu katika nchi yetu, tunu ambayo tumekuwa nayo kwa muda mrefu.

Imetolewa na



Mathew P.M. Mwaimu (Jaji Mstaafu)

Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

05 Februari, 2020